



JATU PUBLIC LIMITED COMPANY

SAFARI YA JATU KURINGIA SOKO LA HISA

2016 ~ 2020



Jenga Afya Tokomeza Umaskini

Yaliyomo

MWANZO WA SAFARI YA JATU	04
LENGO KUU LA JATU KUSAJILIWA	05
CHANZO CHA JATU PLC KUINGIA SOKO LA HISA	05
WALEZI WA JATU PLC	06
USAJILI RASMI WA JATU NA MCHAKATO WA DSE	07
BIASHARA YA JATU PLC	08
MASHAMBA YA JATU PLC	09
VIWANDA VYA JATU PLC	10
SOKO LA BIDHAA ZA JATU PLC	11
JATU KUINGIA SOKO LA HISA	12
JATU IKIWA SOKO LA HISA	13
ELIMU NA MFUMO WA KUNUNUA NA KUUZA HISA ZA JATU KUPITIA DSE	14
MFUMO WA UONGOZI WA JATU PLC	15
MALENGO NA AHADI YA UONGOZI WA JATU KWA WANAHISA	16
SHUKRANI	17



JATU kirefu chake ni Jenga Afya Tokemeza Umaskini. Ni kampuni ya umma iliyosajiliwa tarehe 20.10.2016 na inatambulika kwa nambari ya usajili 130452 na TIN 132-718-008.

Mawasiliano

PSSSF HOUSE Ghorofa Namba 1, 4, 6, 8, 10 na 11

Mtaa wa Samora Morogoro Road, Ilala CBD

S.L.P 42155, Dar es Salaam

Barua pepe info@jatu.co.tz

Simu +255 758 396 767

Tovuti www.jatu.co.tz
www.jatukilimo.com

MWANZO WA SAFARI YA JATU

Kabla ya JATU Plc kusajiliwa ilikuwa ni mradi ndani ya shirika lisilo la kiserikali (NGO) inayojulikana kwa jina la Legal protection and life improvement organization (LPLIO). LPLIO ilianzishwa mwaka 2015 kwa lengo la kutetea haki za binadamu na kupambana na umaskini katika jamii ya Tanzania. LPLIO ilifanikiwa kuwa na wanachama Zaidi ya 200 ambao walikuwa tayari kuanzisha mradi mkubwa wa kiuchumi ili waweze kujikwamua kutoka kwenye umaskini kama lengo la LPLIO lilivyokuwa linasema. Mwanzoni mwa mwaka 2016 JATU ilianzishwa kama mradi wa kudumu kwa wanachama wa LPLIO na mradi huu ulipoanza taratibu za kisheria zilizhitaji mradi huu uweze kuwa kampuni ya biashara inayojitegemea na hivyo kulazimu mradi huu kutoka kwenye NGO ya LPLIO na kusajiliwa kama kampuni ya umma yenye lengo la kujenga afya na kutokomeza umaskini kwa wale waliokuwa wanachama wake pamoja na wengine watakao taka kujiunga na JATU.



LENGO KUU LA JATU KUSAJILIWA

Lengo kuu la JATU kusajiliwa kama kampuni ya Umma ilikua ni kuwapa nafasi watu wengi katika jamii kuchangia mtaji kwa kununua hisa ili kuwa sehemu ya umiliki wa kampuni., pia kuruhusu wawekezaji wa kawaida kushiriki katika miradi shirikishi chini ya usimamizi wa JATU ili waweze kutokomeza umaskini.



CHANZO CHA JATU PLC KUIINGIA SOKO LA HISA

Viongozi wa JATU PLC, Ndugu Peter Isare na Bwana Mohamed Issa Simbano wakiwa bado chuoni, kama wanafunzi wa shahada ya sheria katika chuo kikuu cha Dar es salaam wakiwa na lengo na nia ya kuipeleka JATU soko la hisa, walishiriki shindano la masoko ya mitaji na dhamana lililondaliwa kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi ya elimu ya juu, shindano ambalo liliandaliwa na mamlaka ili kuongeza uelewa kuhusu masuala ya mitaji na masoko ya dhamana. Shindano hilo lilianza rasmi tarehe 5 July, 2016. Ushiriki wao katika shindano hili uliwapu upeo mkubwa sana kuhusu maswala ya mitaji na soko la hisa na hivyo wakagundua kupitia mamlaka ya mitaji na masoko ya umma (CMSA) na soko la hisa la Dar es salaam (DSE) waliokuwa wanachama wao wa LPLIO wanaweza kuwa wawekezaji rasmi katika kampuni kwa kununua hisa na kutambuliwa kisheria, na huu ukawa ndo mwanzo wa JATU PLC kuanza mchakato wa kuorodhesha hisa zake katika soko la hisa.



WALEZI WA JATU PLC

JATU ni zao la vijana wabunifu waliotelewa na ofisi ya waziri mkuu baada ya wazo la JATU kushiriki katika maonesho ya wiki ya vijana mkoani Simiyu kwa udhamini wa ofisi ya waziri mkuu, Idara ya vijana mwaka 2016. Katika shindano hili ambalo lilikua limelenga kuibua vijana wenye mawazo ya ubunifu nchini Tanzania, JATU ilifanikiwa kuwa kumi bora kwa mwaka 2016 na tangu hapo ofisi ya waziri mkuu wamekua walezi wa kudumu wa kampuni hii na hata kuiunganisha JATU na wizara ya kilimo ambayo kupitia mkakati wa sera ya vijana wameiwezesha JATU kushiriki vyema katika miradi ya kilimo na viwanda nchini Tanzania.



Katika Wiki ya Vijana Tar 14.10.2016 Mkoani Simiyu Banda la Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Vijana

USAJILI RASMI WA JATU NA MCHAKATO WA DSE

Mnamo tarehe 20. 10. 2016 safari ilianza rasmi ambapo, JATU PLC ilisajiliwa kama kampuni ya umma na mamlaka ya usajili wa makampuni Tanzania (Brela). Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuwatafuta walezi waelekezi ambao watafanikisha mchakato kwa mujibu wa masharti na kanuni za mamlaka ya masoko na mitaji (CMSA). Tulifanikiwa kuingia mkataba na Archco Financial LTD kama nominated advisor (NOMAD) wetu, hawa waliweza kutushauri na kutuelekeza taratibu zote za kisheria ambazo tulipaswa kuzifuata ili kufanikisha mchakato huu.

Kwa kuwa hatukuwa na mtaji wa kutosha na biashara haikuepo ya kueleweka, tulisaidiana na ARCHCO kutengeneza mpango wa biashara wa kampuni ya JATU. Mchakato ambao ulichukua takribani miezi sita hadi kukamilika. Wakati tunaendelea kuandika mpango kazi huu tuliendelea kujenga kampuni kwa kuanzisha miradi mbali mbali ya kiuchumi ili kutengeneza biashara yetu. Hata hivyo ikumbukwe kwamba mara ya kwanza JATU ilikuwa ni mradi ndani ya shirika lisilo la kiserikali liljulikanalo kwa jina la Legal protection and life improvement organization (LPLIO). Kupitia LPLIO JATU iliweza kupata wanachama ambao walichangia mtaji wa awali wa kuanzisha biashara ya uzalishaji wa bidhaa na hawa ndio wanaoitwa wanahisa waanzilishi wa kampuni ya JATU PLC kama walivyoorodheshwa kwenye kiambatanisho nyuma ya hii Makala.



BIASHARA YA JATU PLC

Baada ya kukusanya mtaji kutoka kwa wanachama wetu tulianza kuzalisha bidhaa ya unga wa dona na sembe. Tulianza kwa kukodi mashine maeneo ya Ukonga Kivule kwa takribani mwaka mmoja baadae tukaamua kuhamishia kituo cha uzalishaji kibaigwa Dodoma ambapo tulifunga mashine za kusaga unga wa mahindi na kukamua mafuta ya alizeti.

Kutokana na kituo cha kibaigwa tuligundua kwamba hatuwezi kuzalisha bidhaa na kuziua bei nzuri kama tutaendelea kutegemea mazao (malighafi) ambayo tunanunua kutoka kwa madalali wa sokoni na ukizingatia kauli mbiu yetu ni jenga afya tokomeza umaskini. Hivyo tulipendekeza kwa wanachama wetu tuanzishe miradi ya kilimo ambayo itatusaidia kupata malighafi kutoka kwa wakulima moja kwa moja ili kuwaepuka madalali wa mazao. Wanachama wetu waliweza kukaa kikao cha tarehe 14.02.2017 na kukubaliana kwamba JATU ianzishe miradi ya kilimo mikoani na wanachama waweze kumiliki mashamba na kampuni iwe na wataalamu watakao saidia kusimamia zoezi lote kuanzia hatua ya awali hadi kuvuna na kwamba mazao hayo yatanunuliwa na kampuni kwa bei elekezi ya soko isiyu na udalali.



DIAMOND FINANCIAL SERVICES
Certified Public Accountants

Financial Advisor and Firm, Member of IFA
Chartered Accountants (Members) Institute
P.O. Box 2200 Dar es Salaam
Tanzania
Phone: 022 253 2200 / 0224 382900
Fax: 022 253 2200 / 0224 382900
E-mail: dfs@diamondfinancial.com

MAFURU & CO. ADVOCATES

NOTARIES PUBLIC AND COMMISSIONER FOR OATHS
(TRADE MARK, SERVICE MARKS AND PATENT AGENTS)

IPS Bldg, 5th Floor
Samora Avenue /Azikiwe Street
P.O. Box 7816
Dar es Salaam,
Tanzania

Tel: +255 22 - 2129542
Fax: +255 22 - 2129543
Call: +255 754 - 286 476
Call: +255 715 - 286 476
Call: +255 715 - 286 476



MASHAMBA YA JATU PLC



Mashamba ya awali yalianzishwa katika mkoa wa Manyara wilaya ya Kiteto ambapo hadi sasa JATU inaendesha mradi mkubwa wa kilimo cha mahindi na alizeti. Baadae tuliendelea kupanua uwekezaji wa kilimo katika mikoa mingine na hadi kufikia sasa tumefanikiwa kuanzisha miradi ya kilimo katika mkoa wa Morogoro wilaya ya kilombero kwa zao la mpunga, mkoa wa Tanga katika wilaya ya Kilindi kwa zao la Maharage, wilaya ya Handeni zao la machungwa, mkoa wa Njombe ni zao la Parachichi, mkoa wa Ruvuma wilaya wa Madaba ni zao la viazi lishe na katika mkoa wa Singida ni zao la Kitunguu.

Mkakati wa kuanzisha mashamba katika mikoa mingine ni mkakati endelevu unaolenga kuhakikisha kwamba kampuni inakuwa na mashamba kila wilaya ili kurahisisha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda ambavyo kampuni huanzisha karibu na maeneo ya mashamba.



VIWANDA VYA JATU PLC



Hadi kufikia sasa kampuni ya JATU imefanikiwa kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao katika mikoa ambayo kuna mashamba ya wanachama kama vile; Kilombero Morogoro ambapo tunazalisha mpunga na kuandaa mchele safi wa JATU PLC, eneo la Kibaigwa ambapo unga wa dona na sembe huzalishwa, lakini pia mafuta ya alizeti. Pia kampuni imeanzisha kituo cha kuzalisha maharage katika wilaya ya kilindi mkoani Tanga.



www.jatu.co.tz

SOKO LA BIDHAA ZA JATU PLC



Kuanzishwa kwa mashamba na viwanda vya kampuni inalenga kuhakikisha kwamba soko la bidhaa za chakula linakuwa nafuu na bora Zaidi, kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano kampuni imefanikiwa kutengeneza mfumo wa masoko ambao unamuwezesha mteja kujisajili na kuwa mwanachama mteja wa kudumu ambaye muda wowote huweza kununua bidhaa za kampuni kupitia simu yake ya mkononi na bidhaa hizo kufikishwa kwa mteja moja kwa moja. Mfumo wa masoko unaotumiwa na kampuni ni wa kisasa rahisi na wa gharama nafuu sana, lakini pia kampuni inatoa nafasi kubwa sana kwa wasambazaji wa bidhaa kuutumia wakiwa kama mawakala wanaosambaza bidhaa kwa wanachama na wateja wa JATU. Ni kutokana na huu mfumo kampuni imefanikiwa kuanzisha maduka ya kusambaza bidhaa yanayofanana kama supermarket.

Supermarket hizi zinaendelea kujengwa nchi nzima na hadi kufikia sasa tumefanikiwa kwa mkoa wa dar es salaam, Arusha, Mtwara, Dodoma na mwanza. Mteja wetu katika mikoa hii anaweza kufika katika ofisi zetu na kujipatia bidhaa bora za JATU au akaingia katika simu yake ya kiganjani na kuweka oda kupitia application ya JATU market na wasambazaji wa kampuni wakamfikishia mteja hizo bidhaa hadi nyumbani kwake.



www.jatu.co.tz

JATU KUNINGIA SOKO LA HISA

JATU ni kampuni ya kwanza ya vijana wa kitanzania inayojishughulisha na mnyororo mzima wa dhamani katika kilimo ambayo inaingia katika soko la hisa la Dar es salaam. Hata hivyo kwa utaratibu wa kawaida JATU ilipaswa kufanya mchakato ujulikanao kitaalam kama Initial public offering (IPO) ili kuweza kuuza hisa zake sokoni kabla ya kusajili na kuorodhesha wanahisa wake. Lakini kutokana na mfumo wa JATU kwamba tayari ilishakuwa na wanahisa waanzilishi ambao wamekidhi vigezo vya kuorodheshwa kwenye soko la hisa na kwa kuzingatia umuhimu wa wanachama hao kuingia katika soko la hisa, ili waweze kuuza hisa zao na wengine kununua hisa za JATU, kampuni kwa kushauriana na wataalamu na mamlaka husika iliama kuanza na hatua hii ya kuorodhesha kwanza wanahisa waliopo katika soko na baadae tutafanya mchakato wa kuuza hisa nyingine zaidi hapo badae kama itahitajika. Bei ambayo hisa moja ya JATU itauzwa kwa siku ya kwanza katika soko la hisa ni shilling 420 za kitanzania na bei hii imekubalika baada ya kufanya mchakato unaojulikana kitaalamu kama share splitting.



JATU IKIWA SOKO LA HISA

JATU ikiwa soko la hisa lengo ni kuwawezesha wanachama wanaotaka kushiriki miradi ya uwekezaji ndani ya JATU wakidhi vigezo vya awali ambapo moja ya kigezo ni kuhakikisha unakuwa na hisa za JATU PLC. Kwa mfano; ili mkulima aweze kushiriki huduma za kilimo zinazoendeshwa na JATU ni lazima awe mwanachama mwenye hisa angalau 200 na hii inategemea na ukubwa wa uwekezaji wake kama inavyobainishwa katika kanuni za ndani za JATU mradi wa kilimo.

Lakini pia ili mtu aweze kuwa mwanachama wakala wa kuuza bidhaa za JATU PLC ni lazima awe na hisa za JATU angalau 200. Hivyo basi kwa kuweka hisa za JATU sokoni wanachama wote wanaolima na JATU na hawakufanikiwa kununua hisa za JATU sasa wanashauriwa na ni lazima kwa mujibu wa kanuni za JATU kilimo waweze kununua na kumiliki hisa za JATU PLC.

Pia wanachama ambao kwa namna moja au nyingine wanahitaji kuuza hisa zao aidha ili wajitoe JATU au kupunguza hisa zao hii ni sehemu sahihi na salama zaidi ya kuuza hisa. Sheria na kanuni za soko la hisa zinamtengenezea mwanahisa njia rahisi za kununua na kuuza hisa zake kupitia soko la hisa.

Katika kipindi chote ambacho JATU itakuwa soko la hisa wanahisa wataweza kufatilia na kuona kwa uwazi utendaji na ukuuaji wa kampuni kwani mamlaka ya masoko ya mitaji imeweka mfumo Rafiki na mzuri zaidi wa kuwafanya watendaji wa kampuni kutenda kwa maslahi na faida za wawekezaji ambao ni wanahisa. Pia kupitia soko la hisa ni rahisi mwanahisa kujua kama thamani ya hisa imepanda au imeshuka kwani kila siku uongozi wa soko hutoa bei za hisa kwa kila kampuni iliyoorodhesha hisa zake. Hali itawawezesha wanahisa wetu kujua thamani ya uwekezaji wao kila muda wanapohitaji kujua.

Uuzaji wa hisa katika soko la hisa huruhusu biashara kupata mtaji na kukuza muonekano wao kwa umma hii itainua na kuikuza kampuni.

Ongezeko la thamani ya kampuni, watu kwa ujumla uheshimu kampuni zilizo orodheshwa kwenye soko la hisa Zaidi ya zile zillizo binafsi/private ambazo hazijaorodheshwa kwenye soko la hisa.

Kwa kampuni yenye uwezo mkubwa wa kukua kama JATU PLC Soko la hisa kwa muda litaongezeka kwa thamani ingawa gharama za hisa za binafsi zinaongezeka na kupanda kila siku nah ii itamfanya mwekezaji kupata faida Zaidi.



ELIMU NA MFUMO WA KUNUNUA NA KUUZA HISA ZA JATU KUPITIA DSE

Kampuni kwa kutambua umuhimu na hali halisi ya wanahisa wake, imeanzisha kitengo maalumu CHA UWEKEZAJI NA MASUALA YA KISHERIA (Investment and legal affairs) ambacho kitawawezesha wanachama kujua elimu sahihi kuhusu hisa na kujua pia taratibu watakazo fuata endapo watahitaji kuuza au kununua hisa za JATU Plc. Kupitia kitengo hichi, elimu itakuwa ikitolewa kwa wanachama kupitia mitandao ya kijamii, makongamano yatakayoendeshwa maeneo mbalimbali ya nchi, mikutano na semina maalumu kupitia ofisi zetu zilizopo nchi nzima.

Lakini pia kampuni imeanzisha application maalumu iitwayo JATU talk, kupitia app hii kampuni itaunda topic maalumu ya somo la hisa na wote wanaohitaji kuendelea kupata elimu ya hisa basi watajiunga na watakuwa wakipata habari hizi kila mara.


JATU talk imeanzisha pia studio maalumu ambayo itafanya mahojiano baina ya wanahisa, wataalamu wa soko la hisa na watu wa kawaida ili kuweza kuhakikisha elimu ya hisa inawafikia watu wengi zaidi na kwa ufanisi.

JATU inaamini kwamba watu wengi wakijua vizuri elimu ya hisa wataweza kushiriki katika miradi mingi jumuishi ambayo gharama ya uendeshaji ni ndogo na faida yake ni kubwa zaidi, na kwa kuwa JATU imejikita katika mazao na bidhaa za chakula, tunaamini kwa kupitia uwekezaji huu wa pamoja kwa kununua hisa tutafikia lengo la kujenga afya na kutokomeza umaskini haraka



MFUMO WA UONGOZI WA JATU PLC

Kampuni ya JATU plc ni kampuni ya kizalendo inayoendeshwa kwa kufuata misingi ya utawala bora, sheria na kanuni zote zinazoongoza kampuni za umma Tanzania, tunao mfumo mzuri unaawahakikishia wanahisa uwakilishi wa moja kwa moja kupitia bodi ya wakurugenzi ambayo imejumuisha makundi yote ya kijamii yaani vijana, wazee, wanawake, wanaume na wenye kipato cha chini ndo watu waliopewa kipaumbele zaidi katika kampuni hii kwani lengo kuu la JATU ni kuhakikisha tunajenga afya na kutokomeza umaskini katika jamii. Katika uongozi wa ndani kampuni imeajiri vijana wenye maono na elimu sahihi ya kuhakikisha kampuni inafanikiwa zaidi katika mipango yake, tunatumia wataalamu katika Nyanja zote kuanzia kilimo, viwanda na masoko. Ufuatao ni muundo wa uongozi katika kampuni ya Jatu;



MAANA YA VIFUPISHO YA MANENO VILIVYOTUMIKA HAPO JUU

- BW**- BODI YA WAKURUGENZI
- MK**- MKURUGENZI MKUU
- MM**- MENEJA MKUU
- MUM** - MKUU WA IDARA YA UTAFAITI NA MIRADI
- MRU**- MKUU WA IDARA YA RASILIMALI WATU NA UTAWALA
- MMUMM**- MKUU WA IDARA YA MAHUSIANO YA UMMA, MASOKO NA MAUZO
- MF** - MKUU WA IDARA YA FEDHA
- MT** - MKUU WA IDARA YA TEHAMA

MALENGO NA AHADI YA UONGOZI WA JATU KWA WANAHISA

Uongozi wa JATU plc unawaahidi wanahisa wake wote waliopo na wale ambao watanunua hisa za JATU kupitia soko la hisa la Dar es salaam kwamba; Kampuni itaendelea kubuni miradi mipya na kuongeza ufanisi zaidi katika miradi yote inayoendelea kwa sasa, tunaahidi kuweka nguvu kubwa katika kuanzisha miradi mingi zaidi ya kilimo maeneo mengi ya Tanzania, tunaahidi kuendelea kuboresha miundombinu yetu ya kilimo na viwanda ili kuweza kuongeza tija na faida katika uzalishaji wetu, tunaahidi kuendelea kuboresha huduma zetu za masoko na bidhaa ili kuwafikia wateja wengi zaidi wa ndani na nje ya Tanzania, tunaahidi kuendelea kuwekeza zaidi katika utafiti na teknolojia ili kuweza kuendana na mabadiliko ya kidunia hasa katika Nyanja ya habari na mawasiliano, tunaahidi kuendelea kuboresha biashara zetu na mahusiano baina ya makampuni na washirika wengine ili kuvutia wawekezaji na wengi zaidi ili tuweze kukuza mitaji na kutatua changamoto zote za kifedha zilizopo kwa wanachama na kampuni kwa ujumla, tunaahidi kuendelea kuwa na nidhamu, busara na hekima katika utendaji wetu siku zote, tunaahidi kuhakikisha kwamba JATU *vision* 2022 inatimia kama ilivyopangwa na kutangazwa mwaka 2018, tunaahidi kuendelea kutoa ajira nyingi zaidi kwa vijana wa kitanzania, tunaahidi kuendelea kuwa wazalishaji na walipa kodi wazuri katika serikali yetu ya jamhuri ya muungano wa Tanzania, na tunaahidi kwamba kampuni hii itaendelea kupanua wigo wake ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha binadamu wote wananufaika na uwepo wa JATU Plc na kwa ujasiri mkubwa kabisa tunaahidi kufanya biashara ya faida na kutengeneza gawio kubwa kwa wanahisa wote. Kwa unyenyekevu mkubwa uongozi wa jatu tunaomba ushirikiano wa jamii nzima ili tuweze kutimiza ahadi zetu kama tulivyoahidi, tunaomba uendeleo kuwa mwanahisa wa JATU na endelea kutukosoa pale unapodhani mchango wako wa kimawazo utaleta mabadiliko chanya katika kampuni.

Wote tutambue JATU ni kampuni ya umma na umma ni sisi sote, jatu itusaidie sisi, JATU iwaisaidie Watoto wetu na vizazi vyote kwa miaka mingi ijayo. Amen.



SHUKRANI

Kampuni inatoa shukrani kubwa kwa waanzilishi wa wazo la JATU chini ya uongozi wa ndugu Peter Isare na Mohammed Issa Simbano, wanachama waanzilishi wote wa JATU, ofisi ya waziri mkuu idara ya vijana, wizara ya kilimo, mamlaka ya masoko na mitaji (CMSA) uongozi wa soko la hisa la dar es salaam (DSE), walezi washauri (NOMAD) Archco Financial limited, uongozi wa chuo kikuu cha Dar es salaam (kitivo cha sharia), taasisi ya LPLIO, taasisi na washirika mbalimbali ambao wameshirikiana na JATU, wanachama waliojiunga na JATU, wateja wa bidhaa za JATU, viongozi wa serikali katika halmashauri mbalimbali ambapo JATU imefika, na serikali kuu kwa ujumla. Lakini kwa heshima ya pekee kabisa kampuni inatoa shukrani za dhati kwa wajumbe wa bodi na wafanyakazi wake wote wanaofanya kazi vituo vyote vya JATU nchini Tanzania. Kwa pamoja tunasema asante na Mungu atubariki katika safari mpya ya soko la hisa ambayo inaanza rasmi tarehe 18.11.2020.





MAWASILIANO

**PSSSF HOUSE GHOROFA NAMBA 6 NA 11
MTAA WA SAMORA
MOROGORO ROAD, ILALA CBD
S.L.P 42155, DAR ES SALAAM**

 info@jatu.co.tz

 +255 758 396 767

 www.jatu.co.tz
www.jatukilimo.com

Pakua sasa

